Namba ya Mtahiniwa: ..............................

# BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

# MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU

## KIDATO CHA PILI

## HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

**060**

**MUDA: Saa 2:30** **Jumatano, 29 Julai 2026 asubuhi**

### Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi (10).
2. Jibu maswali yote.
3. Sehemu A ina alama **kumi na tano (15),** sehemu B ina alama **sabini (70)** na sehemu C ina alama **kumi na tano (15).**
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
5. Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizopewa.
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
7. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAINI YA MKAGUZI** | | |

Shulelibrary.com

Namba ya Mtahiniwa: .............................

## SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kutoka kwenye machaguo uliyopewa kisha andika herufi yake katika jedwali ulilopewa:

(i) Kiperemende ni miongoni mwa watu walioishi katika jamii za asili za Kitanzania kabla ya ukoloni, lakini hakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu jamii aliyokuwa anaishi na namna ilivyoundwa mpaka kuwa jamii kamili. Msaidie Kiperemende kutambua mtiririko wa muundo huo.

A. Lugha, familia na ukoo
B. Familia, kabila na lugha
C. Familia, ukoo na kabila
D. Familia, jamii na ukoo

(ii) Ikemefuna ni kijana wa Kiafrika aliyefanikiwa kupata elimu ya kikoloni wakati wa utawala wao; elimu hiyo haikuwanufaisha Waafrika wenzake kwa sababu ililenga_______________

A. Kueneza upendo kwa Waafrika
B. Kueneza utamaduni na maadili ya Waafrika
C. Kueneza utamaduni na maadili ya kigeni
D. Kuwafanya Waafrika wajue kusoma na kuandika

(iii) Tarehe 10/12/1963 Zanzibar ilipata uhuru wake, Waziri Mkuu akawa Mohamed Shamte. Fikiria kuwa ulikuwa mkazi katika nchi hiyo, ni nani alibaki kuwa kiongozi mkuu wa nchi?

A. Sultan Jamshid bin Abdullah Al Said
B. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere
C. Sultan Sayyid Said
D. Sheikh Abeid Amani Karume

(iv) Maendeleo ya sayansi na teknolojia katika jamii za asili za Kitanzania kabla ya ukoloni yalizidi kuonekana pale binadamu alipovumbua njia ya kuwasha moto kwa kutumia vitu mbalimbali vya asili. Je, ni njia gani miongoni mwa hizi ilitumika?

A. Kwa kutumia kibiriti
B. Kwa kutumia baruti
C. Kwa kutumia vijiti vya ulindi na ulimbombo
D. Kwa kutumia makaa ya mawe

(v) Tanzania imebarikiwa kuwa na fursa nyingi za utalii kupitia urithi wa mbuga za Wanyama. Ukiwa kama mtaalamu wa maliasili, ni aina gani ya urithi iliyokusudiwa?

A. Urithi wa kiutamaduni
B. Urithi unaoshikika
C. Urithi usioshikika
D. Urithi wa asili

Shulelibrary.com

(vi) Babu Kondo aliwasimulia wajukuu wake kuwa, pamoja na mapambano ya awali dhidi ya ukoloni yalipelekea vifo vingi miongoni mwa jamii za kitanzania lakini bado Watanzania walikuwa na ujasiri, uvumilivu na molari ya juu. Hali hiyo ya mapambano ilitokana na___

A. Ukosefu wa chakula na makazi sababu ya vita
B. Harakati za kulinda mali na watu muhimu
C. Matumizi makubwa ya nguvu za giza na miti shamba
D. Uzalendo

(vii) Wamasai ni miongoni mwa jamii ya asili ya Tanzania inayosifika kwa kudumisha mila, desturi na utawala wake mpaka karne ya sasa. Je, ni mfumo upi wa utawala kati ya hizi hutumiwa na jamii hiyo?

A. Mfumo wa kitemi
B. Mfumo wa rika
C. Mfumo wa dola
D. Mfuko wa koo

(viii) Jamii za Kitanzania ni mchanganyiko wa makabila mbalimbali yenye tofauti ya muonekano, asili na tabia. Kutokana na tofauti hizo, jamii hizo zimejigawa katika makundi makuu tofauti tofauti ambayo ni_________________

A. Wabantu, Wahadimu, Wanilo na Wagorowa
B. Wabantu, Wakushito, Wanilo na Wamasai
C. Wabantu, Wakkushito, Wanilo na Wakichembe
D. Wabantu, Wakushito, Wahadimu na Washirazi

Shuleilibrary.com

(ix) Mzee Kurwa alisikika akisema "Tulijaribu kupigana vikali ili kuupinga uvamizi wa kikoloni lakini wakoloni walituzidi nguvu, hatimaye tukashindwa na wakoloni wakapata mwanya wa kuingia katika jamii zetu na kututawala." Unafikiri ni sababu gani ilipelekea kushindwa kwao?

A. Matumizi ya silaha duni miongoni mwa jamii za Kitanzania
B. Ukosefu wa maeneo makubwa ya kupigana vita
C. Ukosefu wa maadili miongoni mwao
D. Matumizi mabaya ya uongozi miongoni mwa viongozi wao

(x) Katika kuimarisha utawala wao, wakoloni walijenga miundombinu mbalimbali ya usafirishaji; ambayo ilikuwa na kazi zifuatazo isipokuwa____________________________

A. Kusafirisha malighafi kwenda bandarini ili kuzipeleka Ulaya
B. Kusafirisha askari wa Kiafrika ili kupigana na wakoloni
C. Kusafirisha bidhaa za viwandani kutoka bandarini kwenda masokoni
D. Kusafirisha maafisa wa kukusanya ushuru/kodi kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha jamii za Kitanzania zilizopigana vita wakati wa uvamizi wa kikoloni katika orodha A na viongozi waliokuwa wanaongoza jamii hizo katika orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika jedwali ulilopewa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| (i) Mapambano ya Wanyamwezi dhidi ya uvamizi wa Wajerumani | A. Mwene Machemba |
| (ii) Mapambano ya jamii za watu wa Pwani | B. Mangi Sina na Mangi Meli |
| (iii) Mapambano ya Wahehe dhidi ya uvamizi wa Wajerumani | C. Mtemi Isike |
| (iv) Mapambano ya Wayao dhidi ya uvamizi wa Wajerumani | D. Chifu Maliare |
| (v) Mapambano ya Wachaga dhidi ya uvamizi wa awali wa Wajerumani | E. Abushir Bin Salum |
| | F. Mtwa Mkwawa |
| | G. Chifu Magere |

| **ORODHA A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **ORODHA B** | | | | | |

**SEHEMU B (Alama 70)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

Shulelibrary.com

3. Mashaka ni mzaliwa na mkazi wa Dar es Salaam Tanzania lakini baba yake ni Msomali na mama yake ni Mshirazi; ambao walihamia kutoka sehemu zao za asili na kuja Tanzania. Fafanua sababu tano zilizopelekea wazazi wa Mashaka kufanya kitendo hicho.
(i) ______________________________
(ii) ______________________________
(iii) ______________________________
(iv) ______________________________
(v) ______________________________

4. Katika harakati za kutafuta uhuru dhidi ya ukoloni nchini Tanganyika na Zanzibar, makundi ya jumuiya, taasisi na vyama mbalimbali vilitumika katika mapambano haya. Kwa kutumia hoja tano madhubuti, eleza makundi hayo:
(i) ______________________________
______________________________
(ii) ______________________________
______________________________
(iii) ______________________________
______________________________
(iv) ______________________________
______________________________
(v) ______________________________
______________________________

5. Fikiria ungekutana na mtu aliyeishi zama za ugunduzi wa chuma akakuelezea athari zilizopatikana baada ya ugunduzi huo. Unadhani ni nukta gani tano muhimu angekueleza?
(i) ____________________
(ii) ____________________
(iii) ____________________
(iv) ____________________
(v) ____________________

6. Mustapha ni mwanafunzi wa kidato cha pili ambaye hana uelewa sahihi kuhusu umuhimu wa mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Wewe, kama mtaalamu wa Historia ya Tanzania, jadili umuhimu wa mapinduzi hayo kwa ufasaha kwa kutoa hoja tano.
(i) ____________________
(ii) ____________________
(iii) ____________________
(iv) ____________________
(v) ____________________

7. Miongoni mwa njia zilizotumika kuitangaza sekta ya utalii nchini Tanzania ni utengenezaji wa filamu ya *´The Royal Tour"*, iliyoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan, ambayo ilionesha maeneo mbalimbali yenye urithi wa asili. Tathmini ni kwa nini maeneo hayo yanapaswa kutunzwa na kila Mtanzania. Toa hoja tano.
(i) ____________________
(ii) ____________________
(iii) ____________________
(iv) ____________________
(v) ____________________

8. Jamii nyingi za Tanzania zilizokuwa chini ya utawala wa wakoloni, ziliishi maisha ya mateso sana kwani wakoloni walilazimisha jamii hizo kufanya kazi ngumu bila malipo yoyote, kulipa kodi kubwa na kupokonywa maeneo yao. Hali hii ilipelekea jamii hizo kuanza kupambana ili kuupinga ukoloni katika jamii zao. Changanua hoja tano za matokeo ya kuupinga uvamizi huo miongoni mwa jamii za Kitanzania.
(i) ____________________
(ii) ____________________
(iii) ____________________
(iv) ____________________
(v) ____________________

9. Mara nyingi Kitufe akitembelea kijijini kwao Kantalamba kila mwisho wa mwaka, hushuhudia michezo ya jadi na ngoma za asili. Kwa kutumia hoja tano madhubuti eleza umuhimu wa uwepo wa tukio hilo kijijini hapo.
(i) ____________________
(ii) ____________________
(iii) ____________________
(iv) ____________________
(v) ____________________

Shulelibrary.com

**SEHEMU C (Alama 15)**

Jibu swali la **kumi (10).**

10. Wakoloni walitumia nguvu kubwa kuharibu maadili ya Kitanzania wakati wa utawala wao, hata hivyo juhudi zao hazikufanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuwa wenyewe walidumisha tamaduni na maadili yao. Fikiria kuwa ulikuwa miongoni mwa walioishi kipindi hicho. Eleza kwa hoja tano maadili yaliyodumishwa.

Shulelibrary.com

Namba ya Mtahiniwa: ..............................

Shulelibrary.com

*Wabillah Tawfiiq*